JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la Pili

JARIDA MAALUM

## UZINDUZI WA MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN






MAMA SAMIA Legal Aid *Campaign*

**KAULI MBIU**
Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo.

**BODI YA UHARIRI**

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
George Mwakyembe | Farida Khalfani | William Mabusi


# HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA KUFIKA HADI VIJIJINI




*Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro akitoa hotuba ya Uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria jijini Dar es salaam Februari 15, 2023.*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa Zanzibar, Mansura Kassim wakiwa pembeni ya nembo na kauli mbiu ya kampeni ya msaada wa kisheria baada ya kuizindua Dar es Salaam Februari 15, 2023. Wengine kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Legal Sevices Facility (LSF) Lulu Ngw'anakilala na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geophrey Pinda na Kulia ni Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Mary Makondo.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro mwenye suti ya bluu, Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria Geophrey Pinda mwenye suti nyeusi, Lulu Ngw'anakilala kutoka LSF wa kwanza kulia na, Mansura Kassim Katibu Mkuu Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala Bora Zanzibar Zanzibar wameshata kitabu cha muongozo wa Kampeni ya Kitaifa ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia. Uzinduzi huo wa kampeni hiyo umefanyika leo Februari 15, 2023 jijini Dar es Salaam..*

**Na Farida Khalfan - WKS Dar es Salaam**

Serikali za Tanzania Bara na Zanzibar Kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo waungana kutekeleza kampeni ya Kitaifa ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayotekelezwa Kwa miaka mitatu kuanzia Februari 2023 hadi Februari 2026.

Kampeni hii itaangalia zaidi upatikanaji haki kwa watu wasiojiweza hususan wanawake na watoto, haya yakiwa ni maagizo ya Rais kuwa kupata haki ni haki ya mwananchi.

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro ameyasema hayo wakati akizindua kampeni hiyo Leo Februari 15, 2023 katika hoteli ya Four Points jijini Dar Es Salaam.

Dkt. Ndumbaro amesema Serikali za Tanzania Bara na Zanzibar na Wadau wa Maendeleo kila mmoja alikuwa anatoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kivyake lakini kuanzia sasa itafanyika kwa pamoja na kufikia ambapo hapakufikiwa mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar.

Dkt. Ndumbaro amesisitiza kuwa " Huu ni mkakati ambao lazima tutekeleze kwa nguvu zote na utagusa maeneo kama kutoa elimu ya haki za Binadamu, kupambana na ukatili wa kijinsia, Masuala ya mirathi, migogoro ya ardhi na mifumo ya Sheria".

Vilevile, Dkt. Ndumbaro amesema Wasaidizi wa Kisheria 4790 kutoka Tanzania Bara na 370 kutoka Tanzania Zanzibar wamepatiwa mafunzo kuhusiana na haki za Binadamu na Msaada wa Kisheria hivyo watakuwa Msaada mkubwa katika kutekeleza kampeni hii kwa ufanisi.

Aidha, Wadau wa Maendeleo wakiwemo GIZ, UNICEF, UNDP na LSF wameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kutekeleza kampeni hii.

Pia Wadau wengine kama TLS, TAWJA, LHRC, TANLAP, CHRAGG na TAWLA wamesema wataendelea kutekeleza Huduma ya utoaji Msaada wa Kisheria ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa kampeni hii.

Naye, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Katiba, Sheria na Utawala Bora Zanzibar Bi. Mansura Kassim amesema kila mdau achukue nafasi yake ili kuona kiini cha uvunjwaji wa haki ikiwemo unyanyasaji kwani vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka badala ya kupungua japokuwa adhabu Kali zimekuwa zikitolewa.

Aidha, akifunga hafla hiyo Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geophrey Pinda amesema jamii inatakiwa iwe wazi na kuzungumza kwa kila kiashiria cha ukiukwaji wa haki ili hatua za haraka za kuzuia zichukuliwe.

Mhe. Pinda ameongeza kuwa kila mwaka kutakuwa na tathmini ya kupima kampeni inavyotekelezwa ili kuona kama Kuna matokeo tarajiwa.

Sheria ya Msaada wa Kisheria ilianza kutekelezwa mwaka 2017 baada ya kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# KATIBU MKUU ZANZIBAR AWATAKA WADAU WA SHERIA KUFANYIA UTAFITI MATUKIO YA UDHALILISHAJI



*Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa Zanzibar, Mansura Kassim akiongea na wadau mbalimbali wa masuala ya kisheria kufanya utafiti juu ya kuendelea kuongezeka kwa matukio mbalimbali ya udhalilishaji*



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe, Dkt. Damas Ndumbaro akimkabidhi Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa Zanzibar, Mansura Kassim, nakala ya Kitabu cha Mwongozo wa Kampeni ya Kitaifa ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia baada ya uzinduzi uliofanyika Dar es Salaam Februari 15, 2023. Wengine kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Legal Sevices Facility (LSF) Lulu Ng'wanakilala na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Geophrey Pinda.*

**Na Farida Khalfan - WKS Dar es Salaam**

Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mansura Mossi Kassim amewataka wadau mbalimbali wa masuala ya kisheria kufanya utafiti juu ya kuendelea kuongezeka kwa matukio mbalimbali ya udhalilishaji licha ya kuwepo kwa sheria kali zinazopinga matukio haya.

Katibu Mkuu ameyasema hayo alipokuwa akihutubia mara baada ya kuzinduliwa kwa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyopewa jina la Mama Samia Legal Aid Campaign yenye lengo la kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa watanzania wanyonge na wenye kipato cha chini ambapo Wizara ya Katiba na Sheria Tanzania Bara na Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Tanzania Zanzibar zinaungana na wadau mbalimbali wa amendeleo pamoja na asasi za kiraia katika kuiendesha kampeni hiyo.

Aidha Katibu Mkuu Mansura aliwataka wadau wa kampeni hii inayotekelezwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kutoa huduma ya msaada wa sheria iliyojikita katika kuangalia vyanzo vya matatizo ambayo yameendelea kuwa sehemu kubwa ya jamii yetu hivyo kampeni hii ya msaada wa kisheria iendane na elimu itakayowawezesha wananchi kujitambua.

Akielezea kwa Upande wa Zanzibar, Katibu Mkuu Mansura alisema hivi sasa kesi ya udhalilishaji visiwani humo adhabu yake ni miaka 30 jela lakini Pamoja na sheria hiyo kuwa kali bado matukio hayo ya udhalilishaji yameendelea kukithiri.

Wananchi wengi wasiokuwa na uwezo hususan maeneo ya vijijini bado hawajafikiwa na huduma ya msaada wa kisheria na elimu ya sheria kiujumla hali hiyo imesababisha Ukatili dhidi ya wanawake na watoto kuendelea kukua katika jamii. Kuwepo kwa nafuu za kisheria hakuwezi kufanywa kuwa kipimo cha upatikanaji wa haki kwa watu wasiokuwa na uwezo, wakati hali ya upatikanaji inaendelea kuathiriwa na mambo ya ndani na nje ya mfumo wa sheria ikiwemo mila na desturi zenye madhara na elimu ndogo ya masuala ya kisheria.

Katibu Mkuu Mansura pia alieleza uimarishaji wa mifumo ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili kwa Zanzibar ni ajenda ya kitaifa. Na dhamira ya Serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa watu wote wanapata haki na kutimiza wajibu kama ilivyoainishwa katika ibara ya 12 hadi 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na kifungu cha11 hadi 25 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia itaongeza uelewa wa kisheria na haki za binadamu kwa jamii na upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa umma katika ngazi ya jamii hususani kwa makundi ya watu wasiokuwa na uwezo na maeneo ya pembezoni. Aidha, itawajengea uwezo wananchi kuzidai na kuzisimamia haki zao zisivunjwe na kufahamu haki na wajibu wao chini ya Katiba na Sheria za nchi.

# ASASI ZA KIRAIA ZAJITOKEZA KWA WINGI KUUNGA MKONO KAMPENI YA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA



Mkurugenzi Mtendaji wa TAWLA Bi. Tike Mwambipile akiongelea umuhimu wa kampeni hii kwa watanzania na namna kampeni hii itavyosaidia upatikanaji wa haki.

**Na George Mwakyembe - WKS Dodoma**

Tarehe 15 ya Mwezi wa Pili mwaka huu, Waziri wa Katiba na Sheria Dkt Damas Ndumbaro alizindua rasmi Kampeni ya Msaada wa Kisheria kwa wanyonge na wale wasioweza kumudu gharama za kupata huduma za kisheria iitwayo Mama Samia Legal Aid Campaign jijini Dar es salaam. kampeni hii imeonekana kuwavutia watu wa makundi mbalimbali zikiwemo asasi za kiraia Tanzania bara pamoja na Tanzania Zanzibar.

Wakiongea kwa nyakati tofauti mara baada ya uzinduzi huo, wadau mbalimbali waliojitokeza kushuhudia uzinduzi wa kampeni hiyo iliyobeba jina la Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan iliyobeba kauli mbiu "Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo" wameonekana kuguswa na kuwa na utayari wa kuhakikisha watanzania wengi waliopo pembezoni na wanyonge wanafikiwa na huduma hii.

*"Hii kampeni imekuja muda muafaka ambapo changamoto zimekuwa nyingi sana, watanzania wengi wanashindwa kumudu gharama kwani sisi wanasheria gharama zetu zipo juu, Kampeni hii itakuwa ni ya kipekee sana na itawasaidia wanawake wengi nchini wenye kipato cha chini kupata haki"* alichangia Mkurugenzi Mtendaji wa TAWLA Bi. Tike Mwambipile.

Kwa upande wake Christina Kamili Ruhinda ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Watoa Huduma za Kisheria Tanzania (TANLAP) alisema wao wapo tayari na wamejiandaa na zoezi la kuendelea kuratibu na kuwajengea uwezo wasaidizi wa kisheria katika kuhakikisha wananchi waliopo pembezoni wanafikiwa na huduma hizo.

Kwa kuangalia umuhimu wa Wasaidizi wa Kisheria (Paral Legal), Wizara pamoja na Asasi za Kiraia wametoa mafunzo kwa Wasaidizi wa Kisheri zaidi ya 4790 kutoka Tanzania bara pamoja na Wasaidizi wa Kisheria 370 kutoka Tanzania Zanzibar kuhusu Haki za Binadamu na Msaada wa Kisheria hivyo watakuwa na msaada mkubwa katika kutekeleza kampeni hii kwa ufanisi mkubwa.



Christina Ruhinda ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Watoa Huduma za Kisheria Tanzania (TANLAP) akielezea utayari wao katika kuratibu na kuwajengea uwezo wasaidizi wa kisheria katika kuhakikisha wananchi waliopo pembezoni wanafikiwa na huduma za msaada wa kisheria.

Wasaidizi wa kisheria hawa wapo mikoa yote nchini na wamekuwa wakipatiwa mafunzo na Asasi za kiraia ambazo zimejikita zaidi katika kutoa huduma ya Msaada wa Kisheria Asasi hizo ni kama vile TLS, TAWLA, LHRC, TANLAP na Asasi zingine zote kwa pamoja zimejipanga kuhakikisha zinatoa huduma ya msaada wa kisheria, lakini pia Asasi hizi zimekuwa zikiratibu mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria juu ya namna gani huduma ya kisheria inatakiwa kutolewa.

Katika kampeni hii, wadau mbalimbali wa Maendeleo nchini kama vile UNICEF, UNDP GIZ, na LSF pia wameunga mkono juhudi za Serikali kuhakikisha kila mwananchi anayehitaji huduma ya msaada wa kisheria basi anafikiwa na kupatiwa huduma za kisheria. Katika huduma hii, Asasi zimekuwa zikiwasaidia wananchi namna ya kutatua matatizo mbalimbali kama vile migogoro ya mirathi, ndoa, ardhi pamoja na migogoro mingine. Asasi hizi zimekuwa zikiwaelekeza wananchi namna ya kutatua migogoro hiyo kwa kufuata sheria pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za kisheria. Kampeni hii ya Huduma wa Msaada wa Kisheria itachangia kuimarisha amani na utulivu na kuongeza kipato cha utengamano wa mtu mmoja mmoja na kuleta utengamano wa kitaifa.

Huduma ya Msaada wa kisheria imekuwa ikifanyika kupitia sheria ya Na.1 ya Mwaka 2017 na Kanuni zake za Mwaka 2018 kwa Tanzania Bara, na Sheria Na.13 ya Mwaka 2018 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2019 kwa upande wa Zanzibar.

# “WADAU TUZUNGUMZE LUGHA MOJA”

## – MHE. PINDA

**Na Lusajo Mwakabuku - WKS Dar es Salaam**




Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Geophrey Pinda akitoa hotuba ya kuhitimisha Uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria jijini Dar es salaam Februari 15, 2023.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geophrey Pinda amewataka wadau wa masuala mbalimbali ya kisheria zikiwemo asasi za kiraia kufanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Katiba na Sheria hasa pale wanapobaini changamoto ambapo baadhi hukimbilia kuziongelea sehemu nyingine zisizo na majibu na kukuza ukubwa wa changamoto hizo.

Pinda alisema kwa sasa serikali imefungua milango na wao wenyewe ni mashuhuda wa jinsi kampeni hii ilivyoandaliwa na ushirikishwaji ulivyokuwa mkubwa kwa taasisi binafsi lengo likiwa ni kuboresha utendaji haki na kuhakikisha huduma ya msaada wa kisheria unamfikia kila mwenye uhitaji na asiyeweza kumudu gharama za wanasheria lakini bila kuhatarisha maadili ya watanzania.

“Leo mmeshuhudia wazi serikali imefungua milango ya sisi kuzungumza na nyie mkiwa na jambo tafadhalini njooni tuzungumze kwanza kabla ya kwenda kupata maoni katika maeneo mengine kwani kufanya hivyo kunaweza sababisha changamoto hiyo kukua zaidi. Naamini sisi na nyie tukizungumza lugha moja na kulinda maadili yetu ni faida kwa watanzania wote kwa ujumla” Alisema Pinda.

Aidha Mhe. Pinda alionesha kufurahishwa kwake na muitikio wa wadau mbalimbali waliojitokeza katika uzinduzi wa kampeni hiyo na kusema ni mwanzo mzuri. Pia akaahidi kuwa kwa kuwa kampeni hii ni ya miaka mitatu, kila mwaka utakuwa unapimwa kuona maendeleo yake na kutatua changamoto zozote zitakazokuwa zinajitokeza lengo likiwa ni kuhakikisha kila mhitaji anafikiwa na huduma hii.

Kwa upande wao, wadau wa maendeleo na asasi za kiraia, wameahidi kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa kampeni hiyo ili kuisaidia jamii kupata msaada wa kisheria sambamba na kutambua haki zao za msingi.

“Kampeni hii ni nzuri na itawafikia wananchi wengi Zaidi. Sisi LHRC tunaahidi kushirikiana na wizara katika kutekeleza kampeni hii,” amesema Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Kampeni ya Kitaifa ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia itatekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar kwa ushirikiano wa Wizara zenye dhamana, Taasisi za Kiserikali, Mashirika yanayotoa msaada wa kisheria na wadau wa maendeleo ya jamii.




Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geophrey Pinda na wageni wengine meza kuu wakati akitoa hotuba yake.



Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) akielezea uzuri wa kampeni hii huku akitoa maono yake juu ya kuwafikia wananchi wengi kwani LHRC wanaahidi kushirikiana na wizara katika kutekeleza kampeni hiyo.

# Matukio katika Picha













